

# MWANAFUNZI WA BIBILIA - 8 Injili



## Utangulizi

Neno injili maana yake ni 'habari njema'. Kwa lugha ya Kiingereza neno hilo linatokana na maneno mawili ya Ki-Anglo Saxon 'Mungu'[wema] na 'dua'[habari].

Katika tafsiri ya bibilia kwa lugha ya Kiingereza, usemi usemao, 'Habari Njema', mara nyingine hutumika katika kumaanisha yale mambo yote aliyoyafanya Yesu. Habari njema ni habari za furaha ya wokovu – ni habari za jambo lililotokea litakalo wanufaisha watu wote duniani. Neno la Kiyunani ambalo mara kwa mara linahusishwa na 'injili' au 'habari njema, ni 'euangelion, ambapo kuna neno 'uinjilisti' [kutangaza habari njema za Yesu]. Mwandishi mmoja alielezea chanzo cha umuhimu wa neno hili kwa kusema:

Mara nyingi katika dola ya Warumi kulikuwa na vita kubwa iliyokuwa ikiendelea katika sehemu moja au nyingine ya mipaka yake ya mbali, na watu walioko katika jiji la Rumi wakiwa wameishiwa pumzi kwa kusubiri habari zinazotoka vitani, ili wasikie kama wameshinda au wameshindwa. Kama wameshinda, mjumbe alikuja akikimbia hadi katika jiji la Rumi akishangilia, 'injili, injili, injili'. Kwa usemi huo alikuwa ana maana ushindi. Habari Njema: Wamemaliza vita na wameshinda. Hii ndiyo maana ya injili. Haina maana tu kusukia ya kitu kizuri, au hadithi nzuri, au hata hadithi nzuri ya Mungu, la , ina maana hii, tumepigana mapambano na sasa tunaweza kutangaza ushindi – amani inaweza kuwa ni ya kwetu.... Katika sehemu ya kwanza ya Injili [Marko], mapambano yanaonyeshwa kuwa ni kati ya Mungu na Shetani. Hii ndiyo vita. Mapambano yalikuwa miaka 2000 iliyopita na ushindi umekuwa ni kwa Mungu – mwanzo wa Injili, habari njema ya ushindi. Je hii ilikuwaje? Vita hivi vilipiganiwa wapi? Jibu ni kwamba; ilikuwa ni katika mtu aitwaye Yesu Kristo, ambaye pia alikuwa ni mwana wa Mungu....[kitabu cha David Pawson, 'Come with me through Mark': 2009. Imetumika kwa ruksa]

Wokovu (kutoka katika adhabu ya dhambi; kuingia katika uzima wa milele), ni ahadi kwa wale wanaotubu, kumuamini Yesu, kubatizwa, na kuendelea kumuamini na kumtegemea na kudumu ndani yake. Habari njema imekabidhiwa kwa wafuasi wa Kristo, ambao wanapaswa kuwaambia wengine juu ya huo wokovu, juu ya utakaso, juu ya kusulubishwa kwa Yesu kwaajili ya dhambi zetu, juu ya ufufuo wake kutoka kwa wafu, na juu ya kuzaliwa upya ambako kunaonyesha mwazo wa maisha mapya 'katika Kristo', ambayo yanawezekana kwa kila mwanamume na mwanamke – na hakika kwa kila mtoto pia.

Angalia kwamba kuna utofauti ambao unaweza kuwepo (ambao unaonyeshwa kwa kutumia herufi kubwa ya herufi ya kwanza) kati ya 'Injili' na 'injili'. Ya kwanza yenye herufi kubwa inawakilisha zile Injili nne katika kanuni ya bibilia (Mathayo, Marko, Luka na Yohana, kwa mtiririko huu) ambapo usemi 'injili', una maana ya kiini cha ujumbe wa mitume (mfano Warumi **15:1**; ambapo Paulo anaandika juu ya , 'ujumbe niliouhubiri kwenu....' Injili ya kweli ya kiutumbe pia ipo sehemu njingine ikilinganishwa na 'injili' ya uongo ambayo baadhi yenu mmeigekua; tazama Wagalatia **1:6**)

## Ahadi ya Mwokozi na Mkombozi wa ulimwengu inapatikana katika mfululizo wa kuras za Agano la Kale

Katika kitabu cha Mwanzo **22:15-18**, Mungu anamuahidi muaminifu Ibrahimu kwamba kupitia mbegu yake mataifa yote yatabarikiwa. Wakati ambapo utekelezaje wa awali ni kwa watu wa Mungu wa hapo kale, tunaweza kuona jinsi baraka kwa watu wa mataifa yote zinavyotokea kwa kadiri wokovu kupitia kwa Yesu Kristo unavyoendelea kujulikana ulimwenguni kote. (Tazana pia Wagalatia **3:8** katika Agano Jipya.) Tazama Isaya **9:2, 6-7** ambapo kuzaliwa kwa Yesu kunatabiliwa, na hasa katika Isaya **53**. Vifungu vingine vya Agano la Kale vinaweza kusomwa katika kuonyesha umuhimu wa umasihi kwa mtazamo wa Agano Jipya.

## Yesu Masihi, alipokuja duniani, alidai kutimiza ahadi za Mungu

Tazama Isaya **61:1-2**; Luka **4:16-21**; Mathayo **3:1-2; 4:23**; Marko **1:15; 8:35; 10:29-30**; Luka **2:10; 9:6**. Wafuasi wa Yesu wanatumwa kumtangaza ulimwenguni kote. Ni pale tu baada ya Yesu kuwa ametangazwa hata, 'miisho ya dunia', ndipo mwisho wa dunia utakapokuja. Wakristo wengi leo wanaamini ya

kwamba, kurahisishwa kwa mawasiliano kunakotokana na utandawazi na vyombo vya kisasa na hii ina maana ya kwamba kwa haraka tunakaribia nyakati ambapo injili inatakiwa kutangazwa ulimwengu wote. Pia wanamatazamio ya upinzani kwa kanisa na injilikuongezeka na kufika hatua mpya katila kuongezeka.

Tazama Mathayo **24:14**; Marko **13:10**; **16:15**; Matendo **8:1-4** na mstari **25**; **13:1-4**; **14:21**; **15:7**; **16:9-10**; Warumi **1:1** na mstari **16**; **15:18-20**; 1 Wakorintho **1:17**; **9:12**; 2 Wakorintho **10:16**.

Yesu alifundisha ya kwamba baada ya kifo chake na ufufuo, Roho Mtakatifu atatumwa. Kisha wafuasi watapewa uwezo wa kuitangaza injili ulimwenguni kote. Tazama Yohana **14:16** na **26**; **15: 26-27**; **16:7** na mstari **13-14**.

Pia tazama: Warumi **2:16**; **16:25**; 1 Wakorintho **1:17**; **9:17-18**; Waefeso **3:1-8**; **6:19**; Matendo **20:24**; 1 Wathesalonike **1:5**; **2:2**; Ufunuo **14:6**

Kuna maonyo mawili maalum kuhusu injili. Kwanza, 'injili' nyingine yoyote ni uovu. Pili, tunaambiwa ya kwamba habari njema ya kweli, haitakubalika na kila mtu. La kusikitisha ni kwamba baadhi ya watu wataikataa. Tazama Mathayo **13:1-23**. Baadhi ya watu wataghafirika na kuanguka katika makosa. Tazama Wagalatia **1:6-9**; **2:11-14**; Wakolosai **2:16-18**; 2Wakorintho **11:1-4** na mstari **13-15**.

Mtume Paulo alisema, 'Na ole wangu kama sitaihubiri injili' (1Wakorintho **9:16**) Ni muhimu kwamba Wakristo wawaambie watu wengine juu ya Habari Njema za wokovu. Hatima ya milele kwa wale wote ambao hawajaokolewa inategemeana na Habari Njema, na Wakristo pia wanakosa baraka kubwa wanaposhindwa kuitangaza.

Copyright © Sovereign World Trust, PO Box 777, TONBRIDGE, Kent, TN11 0ZS, UK  
[www.sovereignworldtrust.org.uk](http://www.sovereignworldtrust.org.uk)

**Publishing and Translation History**

First Published in English by Glory to Glory Publications.

Christian Publications International, PO Box 212, Saffron Walden, CB10 2UU - [www.christian-publications-int.com](http://www.christian-publications-int.com)  
Editor Peter Sammons. Contributors Alex Jacob, David M. Moore, Peter Byron- Davies, Greg Stevenson, Peter Sammons  
ISBN English 978-0-9567831-6-5

This Kiswahili translation for Sovereign World Trust by Revd John Y Madinda with permission  
Swahili Edition Published by Sovereign World Trust ISBN - Kiswahili 978-1-908010-12-4